# TAJWID SOMO LA 1: MAANA YA ELIMU YA TAJWID NA KANUNI ZAKE

**Summary:** Katika somo hili utakwend akujifunza maana ya elimu ya tajwid kisheria. Pia utajifunza hukumu ya kusoma tajwid.

## Maana ya Elimu ya Tajwid

Neno "Tajwid" linatokana na neno la Kiarabu جَوَّدَ (jawwada) ambalo kilugha lina maana ya "ufundi," yaani kufanya kitu kwa uhodari au ustadi. Kwa mujibu wa Kishariah, maana ya Tajwid ni kuitamka kila herufi kama inavyotakiwa kutamkwa, kwa kuipa haki yake na sifa zake huku ukifuata hukumu zote za Tajwid.

Katika Qur'an na Sunnah, imehimizwa sana kusoma Qur'an kwa tajwid au tartila. Elimu hii ya Tajwid ilianza zamani toka enzi za masahaba na wakati Mtume Muhammad (s.a.w) akiwa hai. Mtume alikuwa akiwaelekeza masahaba kwa watu maalumu ili wapate kujifunza Qur'an kwa ufasaha. Imepokewa kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenye kupenda kuisoma Qur'an kama vile ilivyoteremshwa basi na asome kwa Qiraa-ah (kisomo) cha ibn Ummi ‘Abd" (imepokelewa na Ibn Majah na Ahmad).

Pia, Allah amesema: "وَرَتِّلِ ٱلْقُرْءَانَ تَرْتِيلًا" ("na soma Qur'an kwa tartila" - kisomo cha utaratibu upasao). Katika kuonesha maana ya neno tartila, 'Aliy Ibn Abi Talib ambaye ni khalifa wa nne baada ya kufariki Mtume amesema: "التَّرتيلُ هُوَ تَجويد الحُروفَ ومَعرِفةِ الوقوفِ" ("Ni kuisoma Qur'an kwa ujuzi wa kutamka herufi ipasavyo na kuwa na ujuzi wa hukumu za kusimama").

### Kanuni Zinazofungamana na Elimu ya Tajwid

1. Ujuzi wa kujua matamshi ya herufi na yanapopotamkiwa na yanavyotamkwa.
2. Ujuzi wa kujua tabia na sifa za herufi.
3. Ujuzi wa kujua namna ambavyo herufi zinabadilika kulingana na mpangilio wa maneno.
4. Kufanya mazoezi ya ulimi pamoja na kurudia rudia.

### Hukumu ya Kujifunza Tajwid

Kusoma Qur'an bila ya Tajwid, yaani kuchunga herufi ipasavyo, ni katika makosa mbele ya maulamaa wa Tajwid. Maulamaa wa elimu hii wanasema kuwa kujifunza Tajwid ni faradhi kifaya (faradhi ya kutoshelezana) kwa kauli za walio wengi. Pia, wapo wanaosema ni faradhi 'ayn (faradhi ya lazima) kwa kila Mwislamu.

Hawa waliosema ni faradhi kifaya wanamaanisha sio faradhi ya lazima kwa wote ila inatosha kwa wachache wakiwa na elimu hii. Kundi hili pia linasema kuwa inapasa kwa msomaji asisome kwa kukosea ijapokuwa hajui hukumu za Tajwid. Yaani, achunge matamshi kama yalivyoandikwa ili asije akatamka vinginevyo na kubadilisha maana.

Mwisho:

Tukutane somo linalofuata utakwenda kujifunza kuhusu herufi saba katika usomaji wa tajwid.

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 2: HERUFI SABA KATIKAUSOMAJI WA QURAN

**Summary:** Katika somo hili utakwenda kujifunza kuhusu herufi saba katika usomaji wa tajwid.

## Herufi Saba

Wataalamu wa Tajwid wanaeleza kuhusu herufi saba za usomaji wa Qur'an. Qur'an imeshuka kwa lugha ya Kiarabu, na Waarabu wenyewe walitofautiana katika lahaja za lugha ya Kiarabu. Lahaja hizi zilikuwa za makabila saba ya Kiarabu yaliyopo Makkah. Hii ina maana kuwa Waarabu walikuwa na makabila saba wakati huo, na ingawa walizungumza Kiarabu, walitofautiana katika maneno, utamkaji, na hata uandishi. Lahaja hizi zilijulikana kama herufi saba za usomaji wa Qur'an.

Lahaja hizi saba ndizo chanzo cha hizi herufi saba. Hili linathibitika katika maneno ya Mtume Muhammad (s.a.w) aliposema: "Jibriyl alinisomea kwa herufi moja, nikaifanyia marudio mpaka akanifundisha nyingine, nikaendelea kumuomba nyinginezo mpaka mwishowe zikawa herufi (lahaja) saba" (Bukhari na Ahmad).

Makabila haya yalikuwa Quraysh, Hudhayl, Thaqiyf, Hawaazin, Kinaanah, Tamiym, na Yemen. Hivyo, Qur'an ilishuka katika lahaja saba kulingana na makabila haya, na kila kabila linasoma Qur'an kwa namna ambavyo lahaja yao inawafanya waelewe. Wakawa watu wanaandika Qur'an kwa namna wanavyoelewa wao kulingana na lahaja ya kabila lao. Hali hii ilifanya usomaji wa Qur'an utofautiane. Mifano ni kama ifuatavyo: "‘alayhim" wengine walitamka "‘alayhimuw," neno "swiraatw" walitamka wengine "zwiraatw" na wengine "siraatw," na "muumin" wengine walitamka "muwmin."

Amesimulia ‘Umar Ibn Al-Khatab kuwa: “Nilimsikia Hishaam ibn Hakiym akisoma Suratul-Furqan tofauti na vile ninavyoisoma na alivyonifundisha Mtume (s.a.w). Nilikaribia kumsimamisha (asiswalishe) lakini nikamvumilia mpaka akamaliza, kisha nikamshika nguo yake shingoni na kumvuta mpaka kwa Mtume (s.a.w) na kusema: "Nimesikia huyu mtu akisoma (Suratul-Furqan) kinyume na ulivyonifundisha." Mtume (s.a.w) akasema: "Mwachie!" Akamwambia (Hishaam): "Soma." Akasoma. Akasema: "Hivi ndivyo ilivyoteremshwa." Kisha akaniambia mimi: "Soma." Nikasoma. Akasema: "Hivi ndivyo ilivyoteremshwa. Hakika Qur'an imeteremshwa kwa herufi saba, hivyo someni iliyokuwa sahali kwenu."

### Kuenea kwa Uislamu na Uhitaji wa Msahafu Moja

Uislamu ulipoenea zaidi, ikaonekana haja ya kuiandika Qur'an katika lahaja moja ili kuepuka makosa katika usomaji. Katika utawala wa Uthman (r.a), kikundi cha maswahaba kilichokuwa kikiongozwa na Hudhayfah bin al-Yamaaniy kilikuja kwa Uthman (r.a) na kumsihi "auokoe ummah wa Kiislamu kabla haujatofautiana juu ya Qur'an." Uthman (r.a) akaamrisha chini ya uongozi wa Zayd bin Thaabit (r.a) nakala za Qur'an ziandikwe na nakala zote zisizo rasmi zichomwe moto.

Lahaja iliyotumika kuandika Qur'an ilikuwa ile ya Kikuraysh, na msahafu ukajulikana kama 'Msahafu wa Uthman'. Nakala hizo zilisambazwa miji mikuu ya Waislamu kama nuskhah (nakala) rasmi, na nuskhah ya asili ikabakishwa kwa Mama wa Waumini Hafsah (r.a). Zayd bin Thaabit alibaki Madina, 'Abdullah bin Swa'ib alitumwa Makkah, Mughiyrah bin Shu'bah alitumwa Syria, Abu 'Abdur-Rahmaan As-Sulamy alitumwa Kufa, na 'Aamir bin 'Abdil-Qays alitumwa Basra.

Baada ya msahafu huu kusambazwa katika dola ya Kiislamu, lahaja zote zisizo rasmi zilipotea. Msahafu huu ndio chimbuko la misahafu tuliyonayo leo. Ingawa kuna tofauti kubwa za kiuandishi kati ya misahafu ya leo na msahafu huu, kwa mfano, msahafu huu haukuwa na nukta kwenye herufi au irabu pia hazikuwepo. Hayo yalifanyika baadaye kadiri Uislamu ulipoenea maeneo mbalimbali ya dunia na ikaonekana ugumu wa kutumia msahafu ule kwa watu wasiokuwa Waarabu.

**Mwisho:**

Tukutane somo linalofuata tutakwenda kujifunza kuhusu aina za viraa katika usomaji wa Tajwid

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 3: AINA ZA VIRAA KATIKA USOMAJI WA QURAN

**Summary:** Katika somo hili utajifunza kuhusu viraa vya usomaji wa Quran. Viraa hivi ni tofauti na herufi saba

## Qira'at Katika Usomaji wa Qur'an

Qira'at au usomaji, au mbinu za usomaji, zimepewa majina kulingana na majina ya maulamaa  wasomaji wa Qur'an kwa mujibu wa usomaji huo. Kila qira'a inapata mamlaka yake kutoka kwa kiongozi maarufu wa usomaji katika karne ya pili au ya tatu hijri ambaye naye aliipokea riwaya yake kupitiaisnad ya wapokezi hadi kwa Maswahaba wa Mtume.

### Qira'at Mutawatir na Mashhur

Viraa vimegawanyika katika makundi makuu mawili. Kwaida tunafahamu kuwa kuna viraa 7, hata hivyo vipo vingine 3 ambavyo sio maarufu. Zingatia usijechanganya kati ya viraa na herufi saba.

1. Mutawatir: Uwasilishaji ambao una isnad thabiti liyosambaa sana (imepokelewa na watu wengi) kiasi cha kuondoa uwezekano wa makosa yoyote na ambayo ina makubaliano.

2. Mashhur: Hizi ni chache kidogo katika uwasilishaji, lakini bado zimeenea kiasi cha kuondoa makosa kwa kiasi kikubwa.

Kuna qira’at 7 za mutawatir na 3 za mashhur:

**Qira’at za Mutawatir:**

1. Nafi' (d. 169/785)
2. Ibn Kathir (d. 120/737)
3. Abu 'Amr ibn al-'Ala' (d. 154/762)
4. Ibn 'Amir (d. 154/762)
5. 'Asim (d. 127/744)
6. Hamza (d. 156/772)
7. al-Kisa'i (d. 189/904)

**Qira’at za Mashhur:**

1. Abu Ja'far (d. 130/747)
2. Ya'qub (d. 205/820)
3. Khalaf (d. 229/843)

Kuna pia baadhi ya usomaji wa "shadhdh", usomaji adimu ambao kwa kawaida hautambuliki.

## Usomaji na Tofauti za Kieneo

Zamani, wasomi sahihi walijifunza qira’at zote 7 au hata 10. Wakati mwingine wangeweza kutumia qira’a moja siku moja na nyingine siku inayofuata. Baadhi ya watu walikuwa na nakala zenye tofauti zilizowekwa ndani yake. Kulikuwa na kijakazi aitwaye Tawaddud wakati wa Harun ar-Rashid ambaye alijua usomaji wote kumi kwa moyo.

Hata hivyo, usomaji huu uligawanyika kulingana na maeneo. Kwa mfano, mwaka 200 AH, Basra ilikuwa inasoma qira’a ya Abu 'Amr na Ya'qub, Kufa ilikuwa inatumia Hamza na 'Asim, Syria ilikuwa inatumia Ibn 'Amir, Makka ilikuwa na Ibn Kathir, na Madina ilikuwa inatumia Nafi'. Misri, ambayo ilikuwa nyumbani kwa Warsh, ilitumia Warsh kwa kiasi kikubwa hadi kuwasili kwa Waturuki. Kisha Hafs ikawa maarufu kwani ilikuwa ndio tofauti iliyotumiwa na Waturuki. Hafs, kwa njia, ni qira’a ya 'Asim, inayotumiwa Kufa. Riwaya ya Warsh ya qira’a ya Nafi’.

Leo, usomaji unaotumiwa sana ni qira’a ya 'Asim katika riwaya ya Hafs, na qira’a ya Nafi’ katika riwaya ya Warsh. Pia inatumika Afrika ni qira’a ya Abu 'Amir katika riwaya ya ad-Duri.

**Aina za usomaji wa qurani:**

Wataalamu wa elimu ya tajweed wamegawa aina za usomaji katika makundi makuu yafuatayo;-

1.At-Tahqiyq huu ni usomaji wa taratibu kwa kuzingatia hukumu za tajwid na kuzingatia maana. Msomaji atasimama panapotakiwa na atapumzika panapotakiwa. Kila herufi itapewa haki yake kulingana na inavyotamkwa.

2.Al-Hadr huu ni usomaji wa haraka kwa kuzingatia hukumu za tajwid. Hapa msomaji atazingatia hukumu zote na anatakiwa awe makini katika kufanya ghunnah. Hapa msomaji anaweza kuvuta kwa kiwango cha chini mada. Yaani kama mada ina haraka 2 mpaka sita anaweza kuishia kwenye mbili.

3.At-Tadwiyr hapa msomaji atasoma qurani kati ya usomaji wa aina mbili tulizozitaja hapo juu. Na huu ndio uso wa kawaida na wengi wa watu watu wanautumia.

**Mwisho:**

Katika somo linalofuata tutajifunza kuhusu umuhimu wa kusoma tajwid

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 4: UMUHIMU WA KUSOMA TAJWID

**Summary:** Katika somo hili utakwend akujifunza kuhusu umuhimu wa kusoma elimu ya tajwid.

## Fadhila na Umuhimu wa Tajwid

Elimu ya Tajwid ina umuhimu mkubwa katika umma wa Kiislamu. Msomaji wa Qur'an kama hatachunga kisomo anaweza kubadilisha maana ya Qur'an kabisa. Hivyo, elimu ya Tajwid ni msingi wa kuchunga maana ya matamshi ya Qur'an katika usomaji.

Tunahitajia imamu mwenye kiraa nzuri kwa sauti pia awe anajua Tajwid na anaitumia ipasavyo. Mtume (s.a.w) amesema: "Kutoka kwa Abu Mas’uud Al-Answaariyy (r.a) amesema: Mtume (s.a.w) amesema: 'Awaswalishe watu yule mwenye kujua Kitabu cha Allah na wakiwa katika kusoma wako sawa, basi mwenye ujuzi zaidi wa Sunnah, na wakiwa kwenye Sunnah wako sawa, basi aliyetangulia Hijra, na wakiwa katika Hijra wako sawa, basi mkubwa wao kwa umri, wala asiswalishe mtu (mwengine) katika nyumba yake wala katika mamlaka yake wala asikae mahali pake pa heshima isipokuwa kwa idhini yake.'"

Watu hupenda kusikiliza kiraa cha mtu anayesoma vizuri kwa sauti na kuchunga hukumu za Tajwid. Mtume (s.a.w) amesema: "Kutoka kwa Abu Musa Al-’Ash’ariyy (r.a) kwamba Mtume kamwambia: 'Ungeliniona jana nilivyokuwa nakusikiliza kisomo chako. Hakika umepewa mizumari miongoni mwa mizumari ya aila ya Daud.'"

Msomaji wa Qur'an atakuwa pamoja na malaika wema wenye kuandika. 'Aaishah (r.a) amesema: Mtume (s.a.w) amesema: "Yule aliyekuwa hodari wa kusoma Qur'an atakuwa pamoja na Malaika Waandishi (wa Allah) watukufu wema, na yule ambaye anaisoma Qur'an kwa mashaka na huku anajitahidi kwa kudodosa atapata ujira mara mbili."

Mwisho:

Katika somo linalofuata utakwenda kujifunza kuhusu makharija al khuruf katika herufi za kiarabu

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 5: MAKHARIJA AL KHURUF

**Summary:** Katika somo hili utakwenda kujifunza kuhusu makharijal khuruf

## Maana ya Makharijul Huruf katika Tajwid

Makharijul Huruf ni mahali pa kutoka kwa herufi wakati wa kutamkwa. Msomaji mzuri wa Al-Qur'an anapaswa si tu kujua sheria za tajwid, lakini pia kuzingatia na kuelewa makhraj (mahali pa kutoka) na sifa za herufi zinazotamkwa.

Wataalamu mbalimbali wa qiraat wana tofauti katika kupanga (kuainisha) Makharijul Huruf, lakini kwa ujumla msingi wake ni sawa.

Kuna makhraj 17 ambayo yameainishwa katika sehemu 5 kama ifuatavyo:

**1. Al-Halqi / Koo (الحلق)**

Kuna makhraj 3 katika koo:

- Koo la Ndani (Pangoni mwa Koo): Herufi أ na ه
  - Mfano: "أَكَلَ" (akala) - alikula.
- Koo la Kati: Herufi ح na ع
  - Mfano: "حَمْدٌ" (hamdun) - sifa njema.
- Koo la Nje karibu na nyuzi za sauti: Herufi خ na غ
  - Mfano: "خَالِقٌ" (khaaliqun) - Muumba.

**2. Al-Lisani / Ulimi (اللسان)**

Kuna makhraj 10 katika ulimi:

- Pangoni mwa ulimi karibu na koo kugusa 'anak tekak' au juu ya nyuzi za sauti: Herufi ق
  - Mfano: "قَلَمٌ" (qalamun) - kalamu.
- Pangoni mwa ulimi kugusa paa la nyuma: Herufi ك

- Mfano: "كِتَابٌ" (kitaabun) - kitabu.

- Katikati ya ulimi kugusa paa la juu: Herufi ي , ج , ش
  - Mfano: "شَمْسٌ" (shamsun) - jua.
  - Mfano: "جَمَلٌ" (jamalun) - ngamia.
  - Mfano: "يَوْمٌ" (yawm) - siku.
- Kielelezo cha ulimi kugusa meno ya juu: Herufi ض
  - Mfano: "ضَرَبَ" (daraba) - alipiga.
- Sehemu ya mbele ya ulimi kugusa fizi za meno ya mbele ya juu: Herufi ل
  - Mfano: "لَبَنٌ" (labanun) - maziwa.
- Sehemu ya mbele ya ulimi kugusa kidogo juu ya makhraj Lam: Herufi ن
  - Mfano: "نَارٌ" (naarun) - moto.
- Sehemu ya mbele ya ulimi kugusa paa la juu kidogo kwa kunyooka: Herufi ر
  - Mfano: "رَبٌّ" (rabbun) - Mola.
- Sehemu ya mbele ya ulimi kugusa chini ya meno ya mbele ya juu: Herufi د , ط , ت
  - Mfano: "تُفَّاحٌ" (tuffahun) - tufaha.
  - Mfano: "طَالِبٌ" (taalibun) - mwanafunzi.
  - Mfano: "دَرْسٌ" (darsun) - somo.
- Sehemu ya mbele ya ulimi kugusa nyuma ya meno ya mbele ya chini: Herufi س , ز , ص
  - Mfano: "صَابِرٌ" (saabirun) - mvumilivu.
  - Mfano: "زَيْتٌ" (zaytun) - mafuta.
  - Mfano: "سَمَاءٌ" (samaa') - anga.
- Sehemu ya mbele ya ulimi kugusa meno ya mbele ya juu kwa kuachia kidogo: Herufi ظ , ث , ذ
  - Mfano: "ذَهَبَ" (dhahaba) - alienda.
  - Mfano: "ثَوْبٌ" (thawbun) - nguo.
  - Mfano: "ظَلَمَ" (zhalama) - alidhulumu.

**3. Asy-Syafawi / Midomo (الشفوي)**

Kuna makhraj 2 katika midomo:

- Mdomo wa chini kugusa meno ya mbele ya juu: Herufi ف
  - Mfano: "فَرَسٌ" (farasun) - farasi.
- Midomo ya chini na juu ikifungwa pamoja: Herufi ب , م , و
  - Mfano: "وَرْدٌ" (wardun) - waridi.

    - Mfano: "مَكْتَبٌ" (maktabun) - ofisi.
    - Mfano: "بَيْتٌ" (baytun) - nyumba.

**4. Al-Jaufi / Pango la Kinywa (الجوف)**

Kuna makhraj 1 katika pango la kinywa:

- Mahali pa kutoka kwa herufi za mad: Herufi ا , وْ , يْ
    - Mfano: "مَادٌّ" (maaddun) - anayepanua.

**5. Al-Khaisyhumi / Pango la Pua (الخيشوم)**

Kuna makhraj 1 katika pango la pua:

- Pango la ndani ya pua kwa herufi za ghunnah: Herufi ن , م na tanwin.
    - Mfano: "مِنْ" (min) - kutoka.
    - Mfano: "يَنْهَونَ" (yanhawna) - wanakataza.

## Hitimisho

Kujua Makharijul Huruf ni muhimu sana kwa kusoma Qur'an kwa usahihi na ufasaha. Sifa za herufi pia zinachangia katika kutamka herufi hizi kwa njia sahihi. Kuelewa makhraj na sifa za herufi ni sehemu muhimu ya tajwid, inayosaidia kuhakikisha usomaji wa Qur'an unafanyika kama ulivyofundishwa na Mtume Muhammad (s.a.w.).

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 6: SIFAT AL KHURUF

**Summary:** hapa utakwenda kujifunza kuhusu sifa za herufi za kiarabu

## Sifat za Herufi katika Tajwid

Sifat za herufi ni moja ya mambo muhimu katika tajwid ya usomaji wa Al-Qur'an. Sifa za herufi ni tabia zinazofafanua hali ya herufi fulani. Kupitia sifa zake, mtu ataweza kutofautisha herufi fulani kulingana na hali yake ya kutamkwa kama vile kuwa na msisitizo, sauti ya kupiga, na kadhalika.

## Umuhimu wa Kuelewa Sifa za Herufi

Kujua sifa za herufi ni muhimu kama nyongeza kwa kujua makhraj. Kwa kuelewa sifa zake, tunaweza kutofautisha matamshi ya herufi ambazo zina makhraj sawa. Zaidi ya hayo, tunaweza kutambua herufi ambazo ni ngumu na nyepesi au herufi zinazotamkwa kwa sauti nene na nyembamba kutokana na sifa zilizopo kwenye herufi hizo. Sifa za herufi pia zinasaidia kuboresha usahihi wa matamshi ya herufi fulani ili kutamkwa kwa usahihi, hasa kwa herufi zinazofanana kama ث (tha) na س (sin), ح (ha) na ه (ha).

## Maoni ya Wanazuoni Kuhusu Idadi ya Sifa za Herufi

Wanazuoni wana tofauti ya maoni kuhusu idadi ya sifa za herufi, lakini maoni yanayokubalika sana ni yale ya Ibn Jazari; yaani kuna sifa 17 za herufi.

## Aina za Sifa za Herufi

Sifa za herufi zinagawanywa katika aina mbili:

#### 1. Sifat Lazimah (لازمه)

Sifat Lazimah ni tabia ya kudumu ambayo lazima iwepo kwa kila herufi katika hali zote, iwe herufi hiyo ina haraka au haina haraka. Sifa hizi pia zinajulikana kama "sifa zinazopingana". Kuna sifa kumi zinazojumuishwa katika kundi hili:

- Hams na kinyume chake Jahr
- Syiddah na kinyume chake Rakhawah (katikati ya sifa hizi mbili inaitwa Tawasut)
- Isti'la' na kinyume chake Istifal
- Itbaq na kinyume chake Infitah
- Idzlaq na kinyume chake Ismat

#### 2. Sifat 'Aridhah (عارضه)

Sifat 'Aridhah ni tabia zinazoibuka na kubadilika kwa herufi ambazo wakati mwingine zipo na wakati mwingine hazipo kulingana na hali fulani kama vile tarqiq (nyembamba), tafkhim (nene), ghunnah, idgham, au ikhfa', urefu au ufupi na kadhalika. Sifa hizi pia zinajulikana kama "sifa zisizopingana". Kuna sifa saba zinazojumuishwa katika kundi hili:

- Safir - Sauti kutoka mdomoni kama inayosokotwa
- Qalqalah - sauti ya kupiga
- Lin - nyororo
- Inhiraf - kuelemea
- Takrir - kurudiarudia
- Tafasysyi - kusambaa
- Istitolah - kirefu

## Maelezo ya Kina ya Sifa za Herufi

#### Hams (همس)

Hams ni sifa ya kuficha; inapotamkwa herufi hii, hewa hutoka kwa urahisi. Herufi zenye sifa ya hams ni ف (fa), ح (ha), ث (tha), ه (ha), ش (shin), خ (kha), س (sin), ك (kaf), na ت (ta).

#### Jahr (جهر)

Jahr ni sifa ya wazi na dhahiri; inapotamkwa herufi hii, hewa haina uhuru wa kutoka. Herufi zilizobaki baada ya hams ndizo zenye sifa ya jahr.

**Syiddah (شدة)**

Syiddah ni sifa ya nguvu; herufi hii inapotamkwa, sauti inazuiliwa kwa nguvu. Herufi zenye sifa ya syiddah ni ء (hamzah), ج (jim), د (dal), ق (qaf), ط (ta), ب (ba), ك (kaf), na ت (ta).

**Rakhawah (الرخاوة)**

Rakhawah ni sifa ya unyofu; herufi hii inapotamkwa, sauti hutoka kwa urahisi. Herufi zilizobaki baada ya syiddah na tawasut ndizo zenye sifa ya rakhawah.

**Tawasut**

Tawasut ni sifa ya kati; herufi hii inapotamkwa, sauti inatoka kwa kiasi. Herufi zenye sifa ya tawasut ni ل (lam), ن (nun), ع (ain), م (mim), na ر (ra).

**Isti'la' (الإستــعلاء)**

Isti'la' ni sifa ya kuinua au kuinuka; inapotamkwa herufi hii, ulimi huinuka kuelekea paa la mdomo. Herufi zenye sifa ya isti'la' ni خ (kha), ص (sad), ض (dad), غ (ghain), ط (ta), ق (qaf), na ظ (zha).

**Istifal**

Istifal ni sifa ya chini; inapotamkwa herufi hii, ulimi hauinuki kuelekea paa la mdomo.

**Itbaq**

Itbaq ni sifa ya kufunga; inapotamkwa herufi hii, ulimi hulengana na paa la mdomo. Herufi zenye sifa ya itbaq ni ص (sad), ض (dad), ط (ta), na ظ (zha).

**Infitah**

Infitah ni sifa ya kufungua; inapotamkwa herufi hii, ulimi hausogei kuelekea paa la mdomo.

**Idzlaq**

Idzlaq ni sifa ya kuteleza au kurahisisha; herufi hii inapotamkwa kwa urahisi na haraka. Herufi zenye sifa ya idzlaq ni ف (fa), ل (lam), م (mim), ن (nun), ر (ra), na ب (ba).

**Ismat**

Ismat ni sifa ya kuzuia; herufi hizi hazitumiki sana katika maneno ya Kiarabu zaidi ya herufi tatu. Herufi zenye sifa ya ismat ni herufi 23 zilizobaki baada ya idzlaq.

**Safir (صفر)**

Safir ni sifa ya sauti kama ya ndege; herufi hizi hutamkwa kwa sauti ya juu na ya kupiga. Herufi zenye sifa ya safir ni ص (sad), ز (zay), na س (sin).

**Qalqalah (قلقلة)**

Qalqalah ni sifa ya kupiga; herufi hizi hutamkwa kwa sauti ya kugonga. Herufi zenye sifa ya qalqalah ni ق (qaf), ط (ta), ب (ba), ج (jim), na د (dal).

**Lin (لين)**

Lin ni sifa ya unyofu na urahisi; herufi hizi hutamkwa kwa unyofu na urahisi. Herufi zenye sifa ya lin ni و (waw) na ي (ya).

**Inhiraf (الإِنْحِرَاف)**

Inhiraf ni sifa ya kuelemea; herufi hizi hutamkwa kwa ulimi kuelemea. Herufi zenye sifa ya inhiraf ni ل (lam) na ر (ra).

**Takrir (تكرير)**

Takrir ni sifa ya kurudiarudia; herufi hii hutamkwa kwa kurudia sauti. Herufi yenye sifa ya takrir ni ر (ra).

**Tafasysyi (تفشي)**

Tafasysyi ni sifa ya kusambaa; herufi hii hutamkwa kwa sauti kusambaa kwenye mdomo. Herufi yenye sifa ya tafasysyi ni ش (shin).

**Istitalah (استطالة)**

Istitalah ni sifa ya kirefu; herufi hii hutamkwa kwa ulimi kurefuka. Herufi yenye sifa ya istitalah ni ض (dad).

### Hitimisho

Kujua sifa za herufi ni muhimu katika kusoma Qur'an kwa usahihi na ufasaha. Kwa kuelewa sifa hizi, tunaweza kuboresha matamshi yetu na kuhakikisha tunasoma kama ilivyofundishwa na Mtume Muhammad (s.a.w). Sifa hizi zinaongeza uelewa wetu wa tajwid na hufanya usomaji wa Qur'an kuwa wenye athari na maana zaidi.

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 7: HARAKA NA IRABU KATIKA LUGHA YA KIARABU

**Summary:** Katika somo hili utakwenda kujifunzakuhusu haraka na irabu katika lugha ya kiarabu

# Haraka na irabu katika lugha ya kiarabu

Katika lugha ya Kiarabu, maneno "haraka" na "irabu" yana maana maalum na zinatumika kuonyesha matamshi sahihi ya herufi. Ingawa maneno haya mara nyingi hutumiwa kwa kubadilishana, yana tofauti ndogo ambazo ni muhimu kuelewa.

### Haraka (حَرَكَة)

Haraka ina maana ya "harakati" au "miondoko." Katika muktadha wa tajwid na sarufi ya Kiarabu, haraka inahusu alama maalum zinazowekwa juu au chini ya herufi ili kuonyesha irabu (vokali fupi) ambazo zinapaswa kutamkwa baada ya herufi hiyo. Kuna aina tatu kuu za haraka:

1. Fatha (فَتْحَة) - inaashiria sauti ya /a/ na huwekwa juu ya herufi.
    - Mfano: كَ (ka)
2. Damma (ضَمَّة) - inaashiria sauti ya /u/ na huwekwa juu ya herufi.
    - Mfano: كُ (ku)
3. Kasra (كَسْرَة) - inaashiria sauti ya /i/ na huwekwa chini ya herufi.
    - Mfano: كِ (ki)

### Irabu (إِعْرَاب)

Irabu ni neno la Kiarabu linalomaanisha "kufafanua" au "kuweka wazi." Katika sarufi ya Kiarabu, irabu ni mchakato wa kubadilisha matamshi ya mwisho ya neno (haraka ya mwisho) kulingana na nafasi yake katika sentensi na kazi yake kisarufi. Irabu inaweza kuashiria majukumu kama vile nomino kuwa katika hali ya nominative, accusative, au genitive. Irabu inaweza kuwa na alama za haraka lakini pia inaweza kuhusisha alama nyingine kama tanwin na sukun.

Irabu ni kama:

### Raf' (رَفْعٌ): Kwa kawaida inaonyeshwa na dhamma (ُ).

### Nasb (نَصْبٌ): Kwa kawaida inaonyeshwa na fatha (َ).

### Jarr (جَرٌّ): Kwa kawaida inaonyeshwa na kasra (ِ).

### Jazm (جَزْمٌ): Inaonyeshwa na sukun (ْ).

### Tofauti Kuu Kati ya Haraka na Irabu

1. Fani ya Matumizi:
    - Haraka: Inaonyesha matamshi ya vokali fupi kwenye herufi zote za neno.
    - Irabu: Inaonyesha mabadiliko ya matamshi ya mwisho ya neno kulingana na nafasi yake katika sentensi na sheria za sarufi.
2. Lengo:
    - Haraka: Inaelekeza matamshi sahihi ya herufi.
    - Irabu: Inaelekeza majukumu ya kisarufi ya neno katika sentensi.

## Sukun katika lugha ya kiarabu:

Sukun (سُكُون) ni alama maalum inayotumiwa katika lugha ya Kiarabu kuonyesha kwamba herufi haina irabu (yaani, haina sauti ya vokali fupi). Kwa hiyo, sukun siyo haraka wala irabu, lakini ni alama ya sarufi inayotoa taarifa maalum kuhusu herufi.

### Alama ya Sukun

Alama ya sukun inaonekana kama mduara mdogo (°) juu ya herufi, na inaonyesha kwamba herufi hiyo inapaswa kutamkwa bila sauti ya vokali yoyote baada yake.

### Mfano wa Sukun

- كْ (k): Herufi "kaf" yenye sukun juu yake inaonyesha kuwa "kaf" inatamkwa bila vokali.
- مْ (m): Herufi "mim" yenye sukun inaonyesha kuwa "mim" inatamkwa bila vokali.

Katika somo linalofuata tutakwend akujifunzakuhusu hukumu za kitajwid za usomaji wa basmallah yaani bismillah.

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 8: HUKUMU ZA KUSOMA BASMALA NA ISTI'ADHA

**Summary:** Katika somo hili utakwenda kujifunza kanuni za usomaji wa isti’adha na basmallah.

## Hukumu ya Basmala na Isti'adha

Tamko la "Bismillahir-Rahmanir-Rahim" hujulikana kama Basmala, na "A'udhu Billahi Minash-Shaytanir-Rajim" hujulikana kama Isti'adha. Matamko yote haya yana hukumu zake za usomaji mbele ya maulamaa wa Tajwid. Allah amesema: "...pindi unaposoma Qur'an, tafuta hifadhi kwa Allah kutokana na Shetani aliye mbali na rehema za Allah" (yaani, anza kusoma kwa Isti'adha).

### Hukumu ya Isti'adha

Pindi utakapoanza kusoma Qur'an na ukataka kuanza na Isti'adha mwanzoni mwa sura, unatakiwa kuleta Basmala kabla ya kuanza sura. Hivyo basi, kutakuwa kumekutana Isti'adha, Basmala, na sura unayotaka kusoma. Hapa katika kusoma kwake kuna hukumu nne kama ifuatavyo:

1. Kukata zote: Kusoma kila moja kivyake kwa kusimama kati ya vitatu hivi. Yaani, utasoma Isti'adha kisha utasimama, halafu utasoma Basmala kisha utasimama na baadaye utaanza sura.
2. Kuunga zote: Kunganisha Isti'adha, Basmala, na sura bila kusimama.
3. Kuunga Basmala na sura: Kusoma Isti'adha kisha utasimama, halafu utasoma Basmala na sura kwa kuunganisha bila kusimama.
4. Kuunga Isti'adha na Basmala: Kusoma Isti'adha na Basmala kwa pamoja kisha unasimama, kisha unasoma sura.

### Hukumu ya Basmala Kati ya Sura Mbili

Inapotokea umemaliza sura moja na unataka kuingia sura nyingine, hapa kuna hukumu zifuatazo:

1. Kukata zote: Kusoma mwisho wa sura, kisha unasoma Basmala, na kisha unasoma sura inayofuata.
2. Kuunga zote: Kuunganisha mwisho wa sura kisha unasoma Basmala, kisha unaanza kusoma sura mpya bila kupumzika.
3. Kuunga Basmala na mwanzo wa sura: Kumaliza sura kisha utasimama, kisha utasoma Basmala pamoja na kuanza sura mpya bila kusimama.

Mwisho:

Katika somo linalofuata tutakwend akujifunza hukumu za NUN sakina na tanwinkatika usomaji wa Quran.

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 9: HUKUMU ZA NUN SAKINA NA TANWIN

**Summary:** Katika somo hili utakwenda kujifunza kuhusu hukumu za kitajwid za nun sakina na tanwin

# Maana ya Nuwn Sakina na Tanwin

Nuwn saakinah ni herufi ya nuwn (نْ) isiyokuwa na i’raab ambayo huthibiti katika kutamkwa, kuandikwa, kusimama, na katika kuunganisha. Tanwin hapa tunazungumzia hasa fatahateni, kasrteni na dhuma ten endapo zitakutana ha herufi nini kifanyike.

Wataalamu wa Tajwid wameeleza hukumu nne pindi nuwn sakina au tanwin zinapokutana na herufi. Hukumu hizo ni:

### 1. الإِظْهَارْ (Al-Idh'har) - Kudhirisha

Maana: Kudhirisha kitu wazi. Katika hukumu za Tajwid, ni kuitoa kila herufi katika makhraj yake bila ya kuwepo ghunnah. Hii hutokea pale nuwn saakinah au tanwin inapofuatiwa na mojawapo wa herufi sita za al-halq (koo) ambazo ni ء, ه, ح, خ, ع, غ.

### 2. الإِدْغَامَ (Al-Idghaam) - Kuingiza, Kuchanganya

Maana: Kuingiza kitu kwenye kitu. Katika hukumu za Tajwid, ni kuingiza herufi saakin kwenye herufi yenye i’raab na kuzipelekea herufi mbili hizi kuwa herufi moja ya pili nzito. Hii hutokea pale nuwn saakinah au tanwin inapofuatiwa na mojawapo ya herufi sita za idgham ambazo ni ي, ر, م, ل, ن, و.

**Sharti za Idghaam**

- Idghaam inafanyika kwenye maneno mawili tu. Herufi ya mwisho ya neno la kwanza iwe na tanwin au nuwn saakinah na herufi ya kwanza ya neno linalofuata iwe ni mojawapo ya herufi za idgham.

**Aina za Idghaam**

1. Idgham Bighunnah: Kuingiza nuwn saakinah au tanwin kwenye herufi za ي, ن, م, و pamoja na kuleta ghunnah inayotokea puani.

2. Idgham Bighayri Ghunnah: Kuingiza nuwn saakinah au tanwin kwenye herufi za ر, ل bila ya ghunnah.

### 3. الإقْلاَبْ (Al-Iqlaab) - Kugeuza

Maana: Kugeuza kitu na kukifanya kuwa kitu kingine. Katika hukumu za Tajwid, ni kuigeuza nuwn saakinah au tanwin kwa kuitamka kama miym (م) pamoja na ghunnah. Hii hutokea pale tu nuwn saakinah au tanwin inapokutana na ب (baa).

#### Mifano

- "أنبئهم" (anbi'uhum)

### 4. الإخْفِاء (Al-Ikhfaa) - Kuficha

Maana: Kuficha kitu. Katika hukumu za Tajwid, ni kuificha nuwn saakinah au tanwin katika herufi za ikhfaa. Hivyo nuwn saakinah au tanwin itatamkwa ikiwa baina ya idh'har na idgham kwa kuipa ghunnah isiyokuwa na shaddah. Herufi za ikhfaa ni: ث, ج, د, ذ, ز, س, ش, ص, ض, ط, ظ, ف, ق, ك.

#### Mifano

- "من تفعل" (min taf'al)

## Mwisho:

**Katika somo linalofuata tutakwenda kujifunza zaidikuhusu idhhar na kuona mifano zaidi.**

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

# TAJWID SOMO LA 10: HUKUMU YA IDHHAR

**Summary:** Katika somo hili utakwenda kujifunza kuhusu hukumu za idhhar na mifano yake.

## Idhhar Katika Tajwid: Umuhimu na Mifano

#### Kanuni za Idhhar

Maana: Idhhar linamaanisha "uwazi" au "udhihirisho." Ni kanuni inayotumika wakati noon sakinah (نْ) au tanween (ً, ٍ, ٌ) inapofuatwa na mojawapo ya herufi sita za halqi, ikileta matamshi ya wazi bila kunaswa au kuunganishwa.

Herufi za Halqi: Herufi sita za halqi zinazochochea Idhhar ni:

- أ (Alif)
- ه (Ha)
- ع (Ayn)

- ح (Ha)
- غ (Ghayn)
- خ (Kha)

**Mifano ya Kina ya Idhhar**

Noon Sakinah (نْ) na Herufi za Halqi

1. أ (Alif)
   - Mfano: مَنْ أَنْزَلَ (Man Anzala)
     - Hapa, noon sakinah inafuatwa na Alif. Noon inatamkwa wazi bila sauti ya pua.
2. ه (Ha)
   - Mfano: عَنْ هَذَا (An Haadha)
     - Katika mfano huu, noon sakinah inafuatwa na Ha. Noon inatamkwa kwa uwazi.
3. ع (Ayn)
   - Mfano: مَنْ عَمِلَ (Man Amila)
     - Noon sakinah inafuatwa na Ayn. Noon inatamkwa kwa uwazi.
4. ح (Ha)
   - Mfano: فَسَتَعْلَمُونَ حِينَ (Fasta'lamoona Heena)
     - Hapa, noon sakinah inafuatwa na Ha. Noon inatamkwa bila sauti ya pua.
5. غ (Ghayn)
   - Mfano: مِنْ غَيْرِكُمْ (Min Ghayrikum)
     - Noon sakinah inafuatwa na Ghayn. Noon inatamkwa kwa uwazi.
6. خ (Kha)
   - Mfano: وَهُمْ مِنْ خَزَفٍ (Wahum Min Khazafin)
     - Noon sakinah inafuatwa na Kha. Noon inatamkwa kwa uwazi.

| Nuwn saakinah نْ | | |
|---|---|---|
| Idhwhaaru nuwni saakinah katika maneno mawili | Idhwhaaru nuwni saakinah katika neno moja | Herufi |
| فَمَنْ أَسْلَمَ | وَيَنْـَٔوْنَ | ء |
| مِنْ هَادٍ | وَأَنْهَٰرًا | هـ |
| مِّنْ عَمَلِهِم | أَنْعَمْتَ | ع |
| فَمَنْ حَآجَّكَ | وَٱنْحَرْ | ح |

Tanween na Herufi za Halqi

1. أ (Alif)
   - Mfano: سَمِيعٌ عَلِيمٌ (Samee'un Aleemun)
     - Hapa, tanween (double dhamma) inafuatwa na Alif. Tanween inatamkwa kwa uwazi.
2. ه (Ha)
   - Mfano: عَلِيمًا حَكِيمًا (Aleeman Hakeeman)
     - Katika mfano huu, tanween (double fathah) inafuatwa na Ha. Tanween inatamkwa kwa uwazi.
3. ع (Ayn)
   - Mfano: قَوْمٍ عَادٍ (Qawmin Aadin)
     - Tanween (double kasra) inafuatwa na Ayn. Tanween inatamkwa kwa uwazi.
4. ح (Ha)
   - Mfano: سَمِيعٌ حَكِيمٌ (Samee'un Hakeemun)
     - Hapa, tanween (double dhamma) inafuatwa na Ha. Tanween inatamkwa bila sauti ya pua.
5. غ (Ghayn)
   - Mfano: عَلِيمًا غَفُورًا (Aleeman Ghafooran)
     - Tanween (double fathah) inafuatwa na Ghayn. Tanween inatamkwa kwa uwazi.
6. خ (Kha)
   - Mfano: عَذَابٍ خَفِيفٍ (Athaabin Khafeefin)

- Tanween (double kasra) inafuatwa na Kha. Tanween inatamkwa kwa uwazi.

| Tanwiyn | | | |
|---|---|---|---|
| Idhwhaaru tanwiynu katika maneno mawili (dhwammataan) | Idhwhaaru tanwiyni katika maneno mawili (kasrataaan) | Idhwhaaru tanwiyn katika maneno mawili (fat-hataan) | herufi |
| رَسُولٌ أَمِينٌ | عَيْنٍ ءَانِيَةٍ | كُفُوًا أَحَدٌ | ء |
| سَلَٰمٌ هِيَ | قَوْمٍ هَادٍ | فَرِيقًا هَدَىٰ | هـ |
| سَمِيعٌ عَلِيمٌ | خُلُقٍ عَظِيمٍ | شَاكِرًا عَلِيمًا | ع |
| عَزِيزٌ حَكِيمٌ | مُلَٰقٍ حِسَابِيَهْ | تِجَٰرَةً حَاضِرَةً | ح |
| عَزِيزٌ غَفُورٌ | مَّآءٍ غَيْرِ | قَوْمًا غَضِبَ | غ |
| كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ | شَيْءٍ خَلَقَهُۥ | أَزْوَٰجًا خَيْرًا | خ |

Mwisho:

Katika somo linalofuata tutakwend akujifunza kuhusu kuhusmu za idgham.

**Mkala hii imeandaliwa Bongoclass. Kupata makala zaidi tembelea website yetu www.bongoclass.com**

Kitabu hiki kina muendelezo kwa ajili ya mafunzo zaidi. wasiliana nasi kupata kitabu kizima